# VISION ZERO

## Kanuni 7 za dhahabu za Kutokomeza Ajali na kuboresha afya katika ulimwengu wa kazi

VISION ZERO
Safety.Health.Wellbeing.

developed by issa








Ajali na magonjwa kutokana na kazi hayatokei kwa bahati mbaya na siyo kwamba hayawezi kuepukika – huwa kuna sababu. Kwa kujenga utamaduni thabiti wa kuzuia, sababu hizi zinaweza kudhibitiwa na hivyo, ajali, magonjwa na athari nyingine kutokana na kazi zinaweza kuzuilika.

“Vision Zero” ni mbinu ya kimageuzi ya kuzuia na inayounganisha mambo muhimu matatu ambayo ni Usalama, Afya na Ustawi katika ngazi zote za ulimwengu wa kazi.

Vision Zero ya ISSA inanyumbulika na inaweza kuendana na vipaumbele mahususi vya usalama, afya au ustawi kwa ajili ya kuzuia vihatarishi katika muktadha wowote. Kwa sababu ya unyumbufu huu, dira hii ina manufaa katika sehemu yoyote ya kazi, kampuni au sekta katika sehemu yoyote duniani.



## Kanuni 7 za Dhahabu za Vision Zero

1. Simamia – Onyesha uwajibikaji
2. Baini hatari – Dhibiti vihatarishi
3. Ainisha Malengo – Andaa Programu
4. Hakikisha Kuna Mfumo wa Usalama na Afya – Jipange Vizuri
5. Hakikisha Usalama na Afya kwenye Mitambo, Vifaa na Mazingira ya Kazi
6. Boresha Ujuzi – Endeleza Umahiri
7. Wekeza katika nguvu kazi – Hamasisha kwa Kushiriki

### Faida za Usalama na Afya kazini

SMazingira Usalama na Afya na yenye afya sio wajibu wa kisheria na wa kimaadili tu, pia yana faida za kiuchumi. Kuwekeza katika usalama na afya katika ulimwengu wa kazi huepusha madhila kwa wanadamu na kulinda rasilimali yetu ya thamani – amabayo ni uimara wa afya, mwili na saikolojia. Aidha, kwa umuhimu wake, usalama katika ulimwengu wa kazi unaleta matokeo chanya kuhusiana na motisha kwa wafanyakazi, ubora wa kazi na bidhaa, sifa ya kampuni, na viwango vya kuridhika vya wafanyakazi, wasimamizi na wateja na hivyo, huleta mafanikio ya kiuchumi.

Utafiti wa kimataifa kuhusu faida za uwekezaji katika kuzuia magonjwa na ajali yanayotokana na kazi unathibitisha kuwa kila dola moja inayowekezwa katika usalama na afya huzalisha faida inayoweza kuwa zaidi ya dola mbili katika matokeo chanya ya kiuchumi. Mazingira ya kazi yenye afya huchangia kuwapo kwa biashara zenye tija.

### Usalama na Afya vinahitaji uongozi

Kuboresha usalama na afya katika kampuni haimaanishi kuongeza matumizi. Kinachotakiwa ni wasimamizi watende kwa ufahamu, waongoze kwa uthabiti na kujenga hali ya uaminifu na mawasiliano ya wazi katika kila ngazi ya kampuni. Utekelezaji wa mkakati wa kuzuia vifo na ajali mahali pa kazi unahitaji mchango na ushiriki kamili wa watendaji mbalimbali katika ngazi ya kampuni. Ni dhahiri kuwa kufanikiwa au kushindwa kwa utekelezaji wa mkakati wa Vision Zero kutaamuliwa na waajiri na watendaji waliojitoa kikamilifu, wasimamizi walio na motisha na wafanyakazi makini.





## Jinsi Mwongozo Huu Ulivyoandaliwa

Ili kuwasaidia waajiri na wasimamizi kuendelea kuboresha hali ya usalama na afya katika taasisi zao kwa kuendana na Vision Zero, ISSA imeandaa zana ya usimamizi kwa vitendo ili kuendeleza utamaduni thabiti wa Usalama na Afya, kwa kuzingatia utafiti wa kina wa hatua bora zaidi za kuzuia ajali, magonjwa na vifo katika ulimwengu wa kazi. Wakati wa mchakato huu, waajiri, watendaji, mameneja, wataalamu wa udhibiti, wawakilishi wa wafanyakazi na wakaguzi wa kazi zaidi ya 1,000 waliulizwa kuhusu mifano bora ya mbinu za kudhibiti vihatarishi mahali pa kazi. Matokeo yake Mwongozo huu wa vitendo na ufanisi ukaundwa kwa Kanuni 7 za Dhahabu.

## Jinsi ya Kutumia Mwongozo Huu

Kila Kanuni ya Dhahabu katika Mwongozo huu ina muhtasari unaofuatwa na mfululizo wa kanuni elekezi na orodhahakiki rahisi. Kwa hiyo, unapoutumia mwongozo huu, unaweza kupima haraka kati ya kanuni hizi 7 za Dhahabu ni ipi imeshatekelezwa katika taasisi yako, unaweza kuboresha wapi au kama unahitaji kufanya marekebisho.

## Jiunge na Kampeni hii

Kwa maelezo zaidi na mifano bora ya utendaji na kujisajili mtandaoni unaalikwa kutembelea tovuti ya Vision Zero (www.visionzero.global) kujiunga na jumuiya ya kimataifa ya Kampuni zinazotekeleza Vision Zero.

Mahali pa kazi salama na penye afya inawezekana.
Timiza Wajibu Wako!

## Tathmini Kanuni za Dhahabu

- ◯ **KIJANI:** **Imetekelezwa kikamilifu**
- ◯ **NJANO :** **Inahitajika kuboreshwa**
- ◯ **NYEKUNDU:** **Inahitaji kuchukua hatua haraka**



# 1 Simamia – Wajibika

## Kuwa kiongozi - peperusha bendera! Mwenendo wako kama kiongozi unaamua kuhusu mafanikio au kushindwa kwa usalama na afya katika kampuni yako.

Kila Mwajiri, Mtendaji na kila Msimamizi anawajibika kuzingatia usalama na afya katika taasisi yake. Ubora wa uongozi si kuamua tu namna ambavyo Usalama na Afya inatekelezwa katika taasisi, lakini pia utakavyofanya uwe wa unavutia, wenye mafanikio na endelevu. Uongozi unahitaji uwazi katika mawasiliano na utamaduni dhahiri wa usimamizi. Uongozi bora unadhihirishwa kwa uwezo wa kutabirika, uthabiti na usikivu.

Watendaji na wasimamizi ni mfano wa kuigwa: wanaongoza kwa mfano. Wanatenegeneza kanuni na kuzitekeleza. Wanahakikisha kwamba kila mtu anazijua kanuni na kuzitekeleza ipasavyo. Ukiukwaji wa kanuni unapaswa kushughulikiwa mara moja - fuatilia mambo yanavyoenda! Kitendo cha kubaini hali hatarishi kinastahili pongezi. Utendaji na ustahimilivu wa Wasimamizi huweka viwango vya utendaji kwa wafanyakazi wengine.

## Je, mambo yakoje katika taasisi yako?

| 1 Ninaonyesha kwa vitendo usalama na afya, ninaweka viwango na kutumika kama mfano wa kuigwa kwa wafanyakazi na wasimamizi wangu. | Tathmini ya kipengee | Tathmini ya Jumla |
|---|---|---|
| Ninawajibika kwa usalama na afya ya wafanyakazi wangu. Ninafahamu hili na ninaukubali wajibu huu. | ○ ○ ○ | |
| Nimeanzisha na kuwasilisha malengo ya Usalama na Afya mahali pa kazi (dhima, kanuni). | ○ ○ ○ | |
| Usalama na Afya ni kipaumbele kwangu – penye wasiwasi ninasitisha shughuli. | ○ ○ ○ | |
| Usalama na Afya ni ajenda ya kipaumbele katika mikutano yote katika taasisi yangu. | ○ ○ ○ | |
| Ninafahamu kuwa ninatumika kama mfano wa kuigwa. Ninafuata kanuni na kutumia vifaa kinga. Ninapoona vitendo visivyo salama, ninaingilia kati mara moja na kuzungumza na mhusika. | ○ ○ ○ | |
| Ninahudhuria fursa za mafunzo kuhusiana na Usalama na Afya mahali pa kazi kwa viongozi na kupata taarifa mpya. | ○ ○ ○ | |

| 2 Umuhimu wa Usalama na Afya unafahamika kwa kila mtu katika taasisi yangu -na tunayazungumza kwa uwazi. | Tathmini ya kipengee | Tathmini ya Jumla |
|---|---|---|
| Tuna kanuni dhahiri za kutuwezesha kufanya kazi kwa usalama. | ○ ○ ○ | |
| Ninahakikisha kwamba kila mfanyakazi anazijua kanuni hizo. | ○ ○ ○ | |
| Ninajadili masuala ya Usalama na Afya na wafanyakazi wangu. | ○ ○ ○ | |
| Wafanyakazi wangu daima wanajua anayewajibika na anayesimamia. | ○ ○ ○ | |
| Ninaomba maoni kutoka kwa wafanyakazi wangu ili kubaini kama ninatimiza wajibu wangu kama mfano wa kuigwa. | ○ ○ ○ | |

| 3 Ninatenda kwa Uthabiti na Kuonyesha Umuhimu wa Usalama na Afya kazini kwangu. | Tathmini ya kipengee | Tathmini ya Jumla |
|---|---|---|
| Kabla mtu yeyote katika taasisi yangu hajachukua majukumu ya uongozi, atapaswa kuhudhuria semina ya uongozi juu ya Usalama na Afya mahali pa kazi. | ○ ○ ○ | |
| Wasimamizi wangu wanajua jinsi Usalama mahali pa kazi ulivyo muhimu kwangu. Kanuni zinatekelezwa kwa usawa na wafanyakazi na wasimamizi wote. | ○ ○ ○ | |
| Ninapongeza hatua sahihi na kushughulikia utovu wa nidhamu kila unapojitokeza. Sivumilii utendaji kinyume na utaratibu au uzembe mahali pa kazi. | ○ ○ ○ | |
| Pia ninasisitiza umuhimu wa Usalama na Afya mahali pa kazi katika taasisi yangu kwa wakandarasi, kampuni tunazofanya nazo kazi, wasambazaji na wateja. | ○ ○ ○ | |

| 4 Ninawekeza katika Usalama na Afya katika taasisi yangu. | Tathmini ya kipengee | Tathmini ya Jumla |
|---|---|---|
| Wafanyakazi wangu wana muda wa kutosha kufanya kazi zao kwa uangalifu na kwa usalama. | ○ ○ ○ | |
| Wafanyakazi wangu wanajua haki na wajibu wa kusitisha kazi ikiwa haiwezekani kufanyika kwa usalama. | ○ ○ ○ | |
| Mara kwa mara mimi na wasimamizi wangu wote tunahakikisha kwamba mbinu salama za kufanya kazi zinafuatwa, kwa mfano wakati wa ukaguzi wa usalama, ukaguzi wa mtambuko na kwa mujibu wa kanuni ya udhibiti wa pande mbili. | ○ ○ ○ | |
| Ninahakikisha kuwa nyenzo za kutosha na bajeti ya fedha zimetolewa kwa ajili ya Usalama na Afya. | ○ ○ ○ | |



# 2 Baini hatari – Dhibiti vihatarishi

**Tathmini ya vihatarishi hutumika kama nyenzo muhimu katika kubainisha hatari kwa wakati na kwa utaratibu na kutekeleza hatua za kuzuia. Ajali, majeraha na viashirio vya ajali vinapaswa kutathminiwa pia.**

Wewe ni mwerevu, unatumia tathmini ya vihatarishi inayokusaidia kutambua vihatarishi kabla ya ajali kutokea na uzalishaji kupungua; hii inakusaidia kutathmini uwezekano wa hatari na pia kuanzisha na kuweka kumbukumbu za hatua za kujikinga zinazohitajika. Ndiyo sababu zana hii inatumika duniani wakati huu.

Ikitelekezwa vizuri, tathmini ya vihatarishi ni muhimu katika kutoa maelekezo yanayotekelezeka kwa wafanyakazi katika taasisi yako. Ni muhimu kutathmini ajali, matukio na viashiria vya ajali zinazotokana na kazi ili kutambua wa mambo muhimu ya kuzingatia au yanayohitaji maboresho.

## Je, mambo yakoje katika taasisi yako?

| 1 Ninahakikisha kwamba tathmini ya vihatarishi inafanyika katika taasisi yangu, inarekodiwa na kuhuishwa mara kwa mara | Tathmini ya kipengee | Tathmini ya Jumla |
|---|---|---|
| Wasimamizi wangu wanajua kwamba wanapaswa kufanya tathmini ya vihatarishi na kudhibiti hatari na vihatarishi vyote. | | |
| Wafanyakazi wangu, Bodi, Afisa Usalama na Afya mahali pa kazi, Daktari wa kampuni na Wataalamu wengine wa Usalama na Afya mahali pa kazi wanahusishwa. | | |
| Nimeanzisha utaratibu wa msingi wa kufanya tathmini ya vihatarishi:<br>1. Kurekodi muundo wa taasisi yangu<br>2. Kubainisha na kufafanua shughuli zinazofanywa<br>3. Kubainisha hatari na vihatarishi vinavyohusiana na shughuli za taasisi yangu<br>4. Kutathmini hatari na vihatarishi<br>5. Kuanzisha hatua za kuzuia<br>6. Kutekeleza hatua za kuzuia<br>7. Kuthibitisha ufanisi wa hatua za kuzuia | | |
| Matengenezo, utunzaji, utambuzi na utatuzi wa changamoto pamoja na shughuli za wakandarasi na makampuni ya nje na hatua za kufuatwa pale inapotokea dharura huzingatiwa pia. | | |
| Tathmini yetu ya vihatarishi pia inajumuisha vipengele vya afya, ikiwa ni pamoja na afya ya akili. Vipimo vya kemikali hatarishi, kelele na mitetemo hufanywa pale inapohitajika. | | |
| Nimeweka vipindi vya kuhuisha tathmini ya vihatarishi. | | |

| 2 Ajali zitokanazo na kazi, viashiria vya ajali na matukio ya hatari huripotiwa, hurekodiwa kitakwimu na kutathminiwa ili kubaini uwezekano wa kufanya maboresho. | Tathmini ya kipengee | Tathmini ya Jumla |
|---|---|---|
| Ninaarifiwa mara moja kuhusu ajali zote zinazotokea mahali pa kazi, viashiria vya ajali, matukio hatarishi na madhara yoyote ya kiafya yaliyotokea kwa wafanyakazi wangu. | | |
| Ajali mahali pa kazi, rejesta ya huduma ya kwanza, viashirio vya ajali na matukio ya hatari yanachunguzwa kwa uangalifu ili kubaini vyanzo na kuchukua hatua stahiki za kuzuia. | | |
| Tunahifadhi takwimu ili kutambua mienendo ya matukio na maeneo yanapotokea. | | |
| Ninajua sababu tatu muhimu zinazosababisha ajali katika taasisi yangu mara kwa mara na madhara ya ajali hizo. | | |
| Matokeo ya uchambuzi huu yamejumuishwa katika tathmini ya vihatarishi na programu za kuzuia na kukinga vihatarishi. | | |
| Ninafahamu kwamba idadi ya viashiria vya ajali na matukio hatarishi yaliyoripotiwa yanaonyesha utamaduni wa uaminifu katika taasisi yangu. | | |

| 3 Tunatumia maarifa tuliyoyapata kutokana na tathmini ya vihatarishi na uchambuzi wa ajali ili kufanya maboresho. | Tathmini ya kipengee | Tathmini ya Jumla |
|---|---|---|
| Mimi binafsi ninachagua baadhi ya hatua za kujikinga na kuzuia zilizowekwa ili kuthibitisha ufanisi wake. | | |
| Matokeo ya tathmini ya vihatarishi hutumika kufanya maboresho ya uendeshaji katika taasisi yangu. | | |
| Maelekezo binafsi yanatekelezwa na Maelekezo ya Kazi yanatayarishwa kwa kuzingatia tathmini ya vihatarishi. | | |



# 3 Ainisha Malengo – Andaa Programu

## Mafanikio katika usalama na afya mahali pa kazi yanahitaji malengo bayana na hatua madhubuti za utekelezaji, ambazo zinapaswa kubainishwa katika programu.

Usalama na Afya mahali pa kazi una sura nyingi. Weka vipaumbele, weka malengo dhahiri ya Usalama na Afya mahali pa kazi katika taasisi yako na jitahidi kuyatekeleza katika kipindi cha muda wa kati - kwa mfano katika mpango wa miaka mitatu.

Kuna njia mbalimbali zinazowezesha kuandaa mpango wenye malengo mahususi yanayotekelezeka: njia mojawapo ni kuweka lengo la kuendelea kupunguza idadi ya ajali, au kubainisha maeneo mahususi ya kuzingatia Usalama na Afya - kama vile uendeshaji wa mitambo, utumiaji wa mitambo ya kunyanyulia mizigo, vifaa kinga, au kupunguza vumbi. Wafanyakazi wako wakigundua kuwa Usalama na Afya zao ni muhimu kwako binafsi na kwamba kuna kitu kinafanywa katika taasisi kuimarisha us Usalama na Afya, utafanikiwa kwa haraka. Unapaswa pia kutoa mrejesho mara kwa mara kuhusu kufikiwa kwa malengo mliyojiwekea.

## Je, mambo yakoje katika taasisi yako?

| 1 Nimeweka malengo thabiti ya usalama na afya. | Tathmini ya kipengee | Tathmini ya Jumla |
|---|---|---|
| Malengo ya taasisi yetu ni pamoja na kujizatiti kuimarisha Usalama na Afya mahali pa kazi. | ○ ○ ○ | ○ ○ ○ |
| Ili kufikia maboresho katika muda mfupi na wa kati, nimeweka hatua madhubuti kuhusiana na Usalama na Afya mahali pa kazi. | ○ ○ ○ | |
| Vilevile, ninakubaliana kuhusiana na malengo binafsi na wasimamizi na wafanyakazi wangu. | ○ ○ ○ | |
| Ninawajulisha kwa wakati wasimamizi, wafanyakazi, wakandarasi, kampuni washirika, wateja na umma kwa ujumla kuhusu malengo ya kampuni yangu na hatua muhimu ya sasa na ya baadaye. | ○ ○ ○ | |

| 2 Ninapanga shughuli madhubuti ili kufikia malengo yangu | Tathmini ya kipengee | Tathmini ya Jumla |
|---|---|---|
| Ninatumia mpango kazi kuanzisha shughuli madhubuti, programu za Usalama na Afya mahali pa kazi na hatua za ziada zinazokusudiwa kusaidia kufikia malengo yangu. Vilevile, ninapanga ratiba itakayoniongoza. | ○ ○ ○ | ○ ○ ○ |
| Ili kuanzisha shughuli, programu za Usalama na Afya, maadhimisho ya Wiki za usalama, Siku za Afya na hatua zilizopangwa, ninagwa majukumu na kuteua wasimamizi wa miradi. | ○ ○ ○ | |
| Ninatoa taarifa mapema kwa Wasimamizi wote, Wafanyakazi, Wakandarasi, Kampuni Washirika, Wateja na Umma kwa ujumla kuhusu shughuli, mipango ya usalama na afya, maadhimisho ya Wiki za usalama au Siku za Afya, na kuwaalika kushiriki. | ○ ○ ○ | |
| Pia ninaalika familia za wafanyakazi wangu kwenye shughuli, mipango Usalama na Afya na maadhimisho ya siku za afya. | ○ ○ ○ | |

| 3 Ninaweka Takwimu za Utendaji ili Kuthibitisha Ufanisi. | Tathmini ya kipengee | Tathmini ya Jumla |
|---|---|---|
| Kwa msingi wa takwimu za utendaji (idadi ya ajali, washiriki wa mafunzo, wageni siku za maadhimisho, mwitikio wa uhamasishaji wa afya), ninapima kukubalika na mafanikio ya malengo kisha ninatoa taarifa ya matokeo kwa wafanyakazi wote. | ○ ○ ○ | ○ ○ ○ |
| Kwa kuzingatia idadi ya ajali, kiwango cha wagonjwa, siku zisizo na ajali na viwango vya afya, ninatathmini ni kwa kiwango gani nimefanikisha malengo ya kampuni yangu. | ○ ○ ○ | |
| Ikiwa matokeo si yakuridhisha, ninarekebisha shughuli zangu na mpango wangu. | ○ ○ ○ | |
| Kadiri niwezavyo, ninalinganisha takwimu muhimu za utendaji wa taasisi yangu na shughuli za taasisi nyingine za ukubwa sawa katika sekta yangu (kuweka ulinganifu). | ○ ○ ○ | |
| Ninawasilisha mara kwa mara matokeo na mafanikio ya malengo kwa wafanyakazi na wasimamizi wangu, kwa mfano wakati wa mikutano ya wafanyakazi au kwa kutumia ubao wa matangazo. | ○ ○ ○ | |



# 4 Hakikisha Kuna Mfumo wa Usalama na Afya – Jipange Vizuri

## Kupanga usalama na afya mahali pa kazi kwa utaratibu maalumu ndani ya taasisi ni wazo zuri. Ina faida na ni rahisi.

Mpango mzuri wa usalama na afya mahali pa kazi, huisaidia taasisi kuwa na uendeshaji bora na rahisi kwa sababu huondoa usumbufu, upotevu wa muda wa uzalishaji na changamoto za kupungua kwa ubora wa bidhaa. Hizi zote ni sababu za wewe kuhakikisha kuwa utaratibu wako wa Usalama na Afya mahali pa kazi unaendeshwa kwa ufanisi – Ina tija!

Kuandaa orodha hakiki kunaweza kusaidia. Taasisi zinazotaka kufanya vizuri, zinapaswa kusimika mfumo ambao unaruhusu uboreshaji endelevu. Mara tu mfumo utakapoimarika, ukaguzi wa ufanisi utaonesha wanaostahili kutapewa cheti cha tuzo na kutambuliwa.

.

## Je, mambo yakoje katika taasisi yako?

| 1 Muundo, majukumu, umahiri, taratibu na michakato - taasisi yangu imejipanga vyema kusimamia na Usalama na Afya mahali pa kazi. | Tathmini ya kipengee | Tathmini ya Jumla |
|---|---|---|
| Nina muundo wa usalama na afya mahali pa kazi unaozingatia umahiri na uwajibikaji. | | |
| Nimebainisha na kuweka majukumu, wajibu na umahiri wa wasimamizi katika usalama na afya na kuwapa maelekezo haya kwa maandishi. | | |
| Tunao wataalamu wa usalama na afya (mhandisi wa usalama, daktari wa kampuni, mwanasaikolojia, mtaalamu wa afya na mazingira na wengineo). Wataalamu hawa wanashiriki kikamilifu na wananishauri mimi na wasimamizi. Kimuundo wanawajibika kwangu moja kwa moja. | | |
| Nimeweka utaratibu nani anaripoti kwa nani na jinsi gani. Pia inahusisha masuala ya usalama na afya katika taasisi. | | |
| Ninahakikisha kwamba tathmini ya vihatarishi na maagizo ya kazi yanahuishwa kila wakati, na kwamba wafanyakazi wangu wanafahamishwa na kuelekezwa mara kwa mara. | | |
| Wawakilishi wa usalama na afya, watoa huduma ya kwanza na wataalamu wa kuzima moto wapo wa kutosha na wanapata mafunzo na elimu endelevu. | | |
| Uchunguzi wa afya za wafanyakazi kulingana na mahitaji ya kazi hupangwa, hutolewa, hutekelezwa na kurejewa mara kwa mara kulingana na mahitaji | | |

| 2 Usalama na afya katika taasisi ni kigezo muhimu wakati wa kujaza nafasi za usimamizi. | Tathmini ya kipengee | Tathmini ya Jumla |
|---|---|---|
| Katika taasisi yangu, kuzingatia na kutekeleza kanuni za Usalama na Afya ni kigezo kwa mtu kuwa msimamizi. | | |
| Kabla ya uteuzi wa msimamizi mpya, mhusika anahudhuria kozi ya Wasimamizi kuhusu Usalama na Afya kazini. | | |
| Nimeanzisha mikutano ya muda mfupi kuhusiana na usalama inayofanywa na Wasimamizi pamoja na wafanyakazi katika idara zao kila siku kabla ya kuanza kazi. | | |
| Wasimamizi wangu hufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa usalama katika maeneo yaliyo chini yao. Utaratibu na usafi unapewa uangalizi maalumu. | | |
| Ninazungumza mara kwa mara na wasimamizi wangu kuhusu majukumu yao ya Usalama na Afya mahali pa kazi na kupitia kama wanakidhi vigezo. | | |

| 3 Utaratibu wa usalama na afya katika taasisi yangu unakidhi kiwango cha matakwa ya kisheria. | Tathmini ya kipengee | Tathmini ya Jumla |
|---|---|---|
| Ninafuatilia maeneo yote mara kwa mara ili kubaini kama mahitaji ya taasisi yanazingatiwa. | | |
| Mimi binafsi ninahudhuria semina za Usalama na Afya kwa ajili ya Wajasiriamali au Wasimamizi wa kampuni. | | |
| Wataalamu wangu wa Usalama na Afya wanahusishwa katika michakato yote ya kufanya maamuzi juu ya Usalama na Afya. | | |
| Nimeanzisha kamati ya Usalama na Afya mahali pa kazi. Kupitia kamati hii, tunajadili mara kwa mara malengo yetu ya Usalama na Afya mahali pa kazi na kupanga ukuzaji wa Usalama na Afya mahali pa kazi katika taasisi yangu. | | |
| Mimi ndiye kiongozi wa kamati ya Usalama na Afya mahali pa kazi. | | |
| Pamoja na wasimamizi, wawakilishi wa wafanyakazi, wawakilishi wa Usalama na Afya mahali pa kazi na wataalam wa Usalama na Afya tunahudhuria mikutano hiyo, ambayo hufanyika angalau kila robo mwaka. | | |
| Tumejizatiti kukabiliana na dharura kupitia mazoezi ya utayari na udhibiti wa moto kulingana na mpango wangu wa Dharura na Uokoaji. | | |
| Ninathibitisha kiwango cha Usalama na Afya mahali pa kazi katika kampuni ninazofanya nazo kazi. | | |
| Tayari nimeanzisha Mfumo wa Usimamizi wa Usalama na Afya mahali pa kazi kwa taasisi yetu na kuthibitishwa utendaji kazi wake kwa kutumia wakaguzi wa nje. Cheti cha ukaguzi huu kipo. | | |



# 5 Hakikisha Usalama na Afya wa Mitambo, Vifaa na Mazingira ya Kazi

**Usalama wa nyenzo za uzalishaji, mitambo na mazingira ya kazi ni muhimu katika kuzuia ajali zinazotokana na kazi. Athari za kiafya zinapaswa kuzingatiwa pia.**

Mikakati madhubuti ya usalama na afya mahali pa kazi inajumuisha hatua za kitaalamu, kitaasisi na binafsi. Hatua za kitaalamu zinapaswa kuchukua nafasi ya kwanza. Kwa hiyo, ni muhimu kuweka mitambo, nyenzo, vifaa na mazingira ya kazi katika viwango vya sasa vya usalama na afya katika ulimwengu wa kazi, na kuondoa au kupunguza madhara ya kiafya. Kwa kawaida, si mara zote inawezekana kutumia teknolojia mpya na za kisasa. Ndiyo maana maboresho yanahitajika.

Ni muhimu manunuzi yazingatie kwanza usalama, na kuwa lazima vifaa vya usalama viwe sehemu ya shughuli yoyote. Ifahamike kuwa ajali nyingi hutokea wakati wa utatuzi wa changamoto, ukarabati au matengenezo. Hii ni kwasababu mara nyingi, muundo na namna vifaa vilivyotengenezwa havizingatiwi katika kazi hizi na pia kwa sababu vifaa vya usalama havizingatiwi au vinashindwa kufanya kazi. Ni jukumu la uongozi kuzuia haya yasitokee.

## Je, mambo yakoje katika taasisi yako?

| 1 Tunahakikisha kwamba viwango vya sasa vya usalama katika ujenzi na/au ununuzi wa nyenzo za uzalishaji, mitambo na vifaa, na katika usanifu wa mae-neo ya kazi vinafikiwa. | Tathmini ya kipengee | Tathmini ya Jumla |
|---|---|---|
| Kwa kushirikiana na kitengo cha Ununuzi, tunaandaa vigezo kwa ajili ya mchakato wa ununuzi kwa kuzingatia mahitaji ya usalama. | ○○○ | ○○○ |
| Ninazingatia mapendekezo ya tathmini ya vihatarishi wakati wa ununuzi. | ○○○ | |
| Ninanunua mitambo na vifaa endapo mtengenezaji au muuzaji anaweza kutoa mwongozo wa uendeshaji na uchambuzi wa vihatarishi kwa vitu ninavyohitaji. | ○○○ | |
| Ninashirikisha wafanyakazi wenye uzoefu, bodi na wataalamu wangu wa Usalama na Afya kama vile Mhandisi wa Usalama na Daktari wa kampuni. | ○○○ | |
| Katika ununuzi wa mitambo na vifaa, ninahakikisha vinakidhi matakwa ya kanuni na viwango vilivyoidhinishwa, na ikiwezekana viwe na nembo ya ithibati ya usalama kutoka shirika huru la ithibati. | ○○○ | |

| 2 Katika uendeshaji wa kila siku wa nyenzo za uzalishaji, mitambo na vifaa, ninahakikisha kwamba vifaa vya usalama vinafanya kazi ipasavyo na vinatumiwa. | Tathmini ya kipengee | Tathmini ya Jumla |
|---|---|---|
| Ninahakikisha kuwa hali ya usalama wa teknolojia inafanyiwa mapitio katika vipindi maalumu. | ○○○ | ○○○ |
| Ninahakikisha kwamba taarifa zilizo katika mwongozo wa matumizi unaotolewa na mtengenezaji zimejumuishwa katika maelekezo ya kazi yanayoeleweka kwa urahisi, na kutumika katika mafunzo na maagizo ya mara kwa mara ya wafanyakazi. | ○○○ | |
| Ninaweka mpango wa ukaguzi na kuteua watu wanaowajibika. | ○○○ | |
| Ninaweka utaratibu wa namna ya kufanya matengenezo, ukarabati na utatuzi wa changamoto kwa sababu shughuli hizi husababisha ajali kwa urahisi. | ○○○ | |
| Ninabainisha matumizi sahihi na salama ya njia (magari, mitambo na watembea kwa miguu) katika eneo la taasisi wakati wote. | ○○○ | |
| Ninahakikisha kwamba njia za kutokea wakati wa hatari pamoja na vifaa vya kudhibiti moto na milipuko vimewekwa katika hali salama wakati wote. | ○○○ | |

| 3 Tunahakikisha kwamba nyenzo za uzalishaji, mitambo na vifaa havisababishi hatari zozote za kiafya, na vihatarishi vyote vimedhibitiwa. | Tathmini ya kipengee | Tathmini ya Jumla |
|---|---|---|
| Ninahakikisha kwamba vumbi, kemikali hatari, kelele na mitetemo imebainishwa na/au kupimwa, kupunguzwa kadiri inavyowezekana na kwamba ufanisi wa hatua za kuzuia zinafanyiwa mapitio katika vipindi maalumu. | ○○○ | ○○○ |
| Nyenzo za kupunguza uchafuzi wa hewa, kama vile mifumo ya kupunguza vumbi, inakaguliwa mara kwa mara na ufanisi wake unathibitishwa. | ○○○ | |
| Tunazingatia usanifu wa ki-egonomia wa maeneo ya kazi na vifaa vya kazi, kama vile mwanga wa kutosha, unyanyuaji salama wa vitu vizito, mkao mzuri na kuepuka mkao usiofaa. | ○○○ | |



# 6 Boresha Ujuzi – Endeleza Umahiri

## Wekeza kwenye mafunzo na ujuzi wa wafanyakazi wako, na hakikisha kwamba maarifa yanayohitajika yanapatikana kila mahali pa kazi.

Katika baada ya ajali, mara nyingi watu huuliza: Ilitokeaje? Vifaa vya kiufundi na mitambo ya uzalishaji inazidi kuwa na tija na kufanya kazi haraka zaidi, lakini pia ni tata kuendesha na nyepesi kuharibika. Hii inaleta umuhimu wa kupeleka watu wenye sifa na waliofunzwa vizuri katika kufanya kazi maeneo ya kazi. Ni wajibu wa Uongozi wa juu kuhakikisha kuwa maelezo ya kina ya sifa zinazohitajika kwa kila nafasi katika taasisi yanabainishwa na kwamba kila mfanyakazi anaweza kutekeleza majukumu ya nafasi yake.

Mahali pa kazi hubadilika kila wakati. Maarifa yanapungua kadri muda unavyoongezeka, na ujuzi wa wafanyakazi unapaswa kuhuishwa mara kwa mara. Zaidi ya hapo awali, kutoa mafunzo na elimu endelevu ni jambo la lazima. Wakati huohuo, ni lazima kujifunza uongozi na usimamizi!

## Je, mambo yakoje katika taasisi yako?

| 1 Tunajua ni sifa na ujuzi gani tunaohitaji ili kudumisha usalama na afya katika teknolojia tunayotumia ili kuepuka vikwazo katika uzalishaji. | Tathmini ya kipengee | Tathmini ya Jumla |
|---|---|---|
| Huamua mara kwa mara vigezo vya kazi mbalimbali vinavyohitajika katika taasisi yangu. | ○ ○ ○ | ○ ○ ○ |
| Tunapoajiri Wafanyakazi wapya, vigezo hivi hupitiwa upya kwa utaratibu na kutayarisha mpango wa mafunzo. | ○ ○ ○ | |
| Ninahakikisha pia kwamba wafanyakazi wanaoacha kazi, wanaandika umahiri wao na kuwapa warithi wao, ili wapitie na kujifunza, kwa mfano, mafunzo yakukabidhiana kazi baina ya wafanyakazi wanaoondoka na warithi wao. | ○ ○ ○ | |
| Ninazingatia uwezekano na kutoa elimu endelevu na sifa za ziada kwa wafanyakazi wangu. | ○ ○ ○ | |

| 2 Ninawekeza katika utaratibu wa mafunzo na elimu endelevu ya wafanyakazi wangu na kusaidia maendeleo yao binafsi. | Tathmini ya kipengee | Tathmini ya Jumla |
|---|---|---|
| Tunabaini mara kwa mara hitaji la mafunzo na elimu endelevu, kwa mfano wakati wa vikao vya kutathimini utendaji, na kuandaa mpango wa mafunzo wa muda wa kati. | ○ ○ ○ | ○ ○ ○ |
| Ninatumia vizuri fursa za mafunzo na elimu endelevu ya Vyuo Vikuu, Vyuo vya Ufundi, Mamlaka za Serikali na Watoa Huduma za Bima ya Ajali, na kuwapeleka wafanyakazi mara kwa mara kwenye kozi za mafunzo. | ○ ○ ○ | |
| Pia ninatumia fursa za elimu endelevu zinazotolewa na Watengenezaji, Wasambazaji na Vyama mbalimbali. Ninatumia pia njia mpya za mawasiliano (Intaneti, Elimu kwa njia ya kielekroni) kuhuisha maarifa na ujuzi. | ○ ○ ○ | |
| Ninazingatia ubora wa hatua za elimu endelevu na kuhakikisha zinajumuisha vipengele vya kujifunza kwa vitendo. | ○ ○ ○ | |

| 3 Ninatumia umahiri wa ziada au mpya wa wafanyakazi wangu na kuwapangia majukumu mapya yanayoendana na umahiri wao. | Tathmini ya kipengee | Tathmini ya Jumla |
|---|---|---|
| Baada ya semina za elimu endelevu, ninazungumza na wafanyakazi wangu na kuwauliza kuhusu maarifa na mawazo mapya waliyopata. | ○ ○ ○ | ○ ○ ○ |
| Ninawawezesha wafanyakazi wanaomaliza elimu endelevu kuwashirikisha wafanyakazi wenzao maarifa mapya waliyopata. | ○ ○ ○ | |
| Nina hakika kwamba elimu endelevu ni muhimu ili kudumisha kiwango cha juu cha Usalama na Afya katika kampuni yangu. | ○ ○ ○ | |

| 4 Maarifa huleta usalama - ndiyo maana ninathamini sana mafunzo ya vitendo na yanayoeleweka kwa wafanyakazi. | Tathmini ya kipengee | Tathmini ya Jumla |
|---|---|---|
| Mafunzo yanatolewa kwa washiriki, yakitumia utaratibu wa majadiliano, badala ya ufundishaji unaofanywa na mtu mmoja. Ninahakikisha mafunzo ya namna hii yanapatikana kwa wasimamizi pia. | ○ ○ ○ | ○ ○ ○ |
| Katika utoaji wa maelekezo na mafunzo tunazingatia hali tofauti ya maarifa na ujuzi wa lugha mbalimbali. | ○ ○ ○ | |
| Ninajiridhisha kuwa wafanyakazi wameelewa Mada. Nina hakikisha maelekezo muhimu na Mafunzo na elimu endelevu yamerekodiwa kwa usahihi. | ○ ○ ○ | |



# 7 Wekeza katika nguvu kazi – Hamasisha kwa Kushiriki

## Wahamasishe wafanyakazi wako kwa kuwashirikisha katika masuala yote ya Usalama na Afya. Uwekezaji huu una tija!

Kuhamasisha wafanyakazi wako kufanya kazi kwa usalama na afya ni mojawapo ya majukumu yako muhimu ya kiuongozi. Taasisi zinazotoa shukrani kwa wafanyakazi wao na kuwashirikisha kikamilifu katika Usalama na Afya zinanufaika na ujuzi, uwezo na mawazo ya wafanyakazi wao.

Wafanyakazi wanaposhirikishwa kutoa maoni, mfano wakati wa kufanya tathmini ya vihatarishi au katika maandalizi ya kanuni naa maelekezo ya uendeshaji, watayatekeleza kwa hiari. Motisha inakuzwa kupitia matukio jumuishi au siku za uhamasishaji ambapo Usalama na Afya vitaonyeshwa kwa vitendo au mifano halisi. Haigharimu chochote kuwasifu wafanyakazi kwa tabia zinazozingatia usalama, kuwauliza juu ya maoni yao, na kupongeza majukumu ya kazi ngumu na pia kushughulikia mara moja vitendo visivyo salama au viashiria vya ajali. Kufanya hivyo kunaweza kutengeneza mtazamo binafsi wa wafanyakazi na kuwahamasisha kufanya kazi kwa usalama na kwa ufahamu na zaidi ya yote, kujiamini.

Lengo ni kila mtu awajali wenzake na pia ajijali yeye mwenyewe - “mmoja kwa wote - wote kwa mmoja!”

## Je, mambo yakoje katika taasisi yako?

| 1 Ninaonyesha kwa vitendo shukrani zangu binafsi kwa wafanyakazi. Vilevile, ninatarajia wasimamizi wote na wafanyakazi waandamizi wafanye hivyo. | Tathmini ya kipengee | Tathmini ya Jumla |
|---|---|---|
| Ninawashirikisha wafanyakazi wangu katika maamuzi yanayohusiana na usalama na afya mahali pa kazi. Ninawapongeza wafanyakazi kwa tabia salama - na kushughulikia tabia isiyo salama mara moja. | | |
| Ninafikiwa kwa urahisi na wafanyakazi wangu na ninaonyesha uwepo wangu katika taasisi. | | |
| Ninapokea taarifa, ripoti kuhusu uharibifu na mawazo ya wafanyakazi wangu kwa uzito, ninahakikisha kuwa utatuzi unapatikana na kutoa mrejesho kwa wakati. | | |

| 2 Ninatumia hoja za Usalama na Afya mahali pa kazi ili kuanzisha na kukuza zaidi utamaduni mzuri ndani ya kampuni. | Tathmini ya kipengee | Tathmini ya Jumla |
|---|---|---|
| Tunadumisha utamaduni wa kampuni unaozingatia uaminifu, heshima na ushirikiano. | | |
| Matatizo yanashughulikiwa kwa uwazi katika taasisi yangu. Kila mtu ana haki na wajibu wa kusitisha kazi endapo kuna hali ya hatari na mazingira yasiyo salama ya kufanya kazi. | | |
| Ninajitahidi kuhakikisha kwamba wafanyakazi na familia zao wanajua kuwa wanafanya kazi katika taasisi inayozingatia usalama. | | |
| Wafanyakazi katika taasisi yangu wanajaliana. | | |
| Ninaalika wafanyakazi wangu, familia zao, wateja na washirika wetu kuhudhuria maadhimisho ya Siku za Afya, Siku za Usalama na Afya mahali pa kazi au kupeana ufahamu juu ya Usalama na Afya mahali pa kazi. | | |

| 3 Katika taasisi yetu, tuna miundo yenye kusaidia wafanyakazi kushiriki na kuwapa motisha. | Tathmini ya kipengee | Tathmini ya Jumla |
|---|---|---|
| Ninatuza utendaji kazi wenye ufanisi na unaozingatia usalama kwa wafanyakazi na wasimamizi kwa motisha za kifedha au nyinginezo. | | |
| Ninawahamasisha wafanyakazi wangu kuchangia mawazo yao kuhusu Usalama na Afya, kwa mfano kupitia sanduku la maoni, ubao wa matangazo au kwa njia ya intraneti. | | |
| Kwa kufanya hivyo, ninatumia pia majukwaa ya mikakati ya Kitaifa na Kimataifa ya Usalama na Afya mahali pa kazi, Kampeni, Zawadi na Tuzo, ambapo ninawasilisha mawazo bora ya wafanyakazi wangu. | | |
| Ninawapa motisha wafanyakazi wangu kuripoti kwa uwazi hatari na viashiria vya ajali na kuwapa zawadi kwa kuwasilisha ripoti hizo. | | |
| Ninasisitiza kuwa mwenendo salama ni hitaji la msingi la kufanya kazi katika taasisi yangu. | | |
| Wafanyakazi wanafahamishwa kuhusu hatari za kiafya zisizoepukika na hatua za kuchukua ili kujikinga. | | |

Jiunge na kampeni hii leo!

**www.visionzero.global**
**#visionzeroglobal**

Mwongozo wa Vision Zero umeandaliwa na Jumuiya ya Kimataifa ya Hifadhi ya Jamii na Tume yake Maalumu ya Kuzuia Ajali na Magonjwa kwa kushauriana na taasisi na wataalamu mbalimbali.

Ijapokuwa uangalifu umezingatiwa katika maandalizi na utayarishaji wa taarifa zilizochapishwa kwenye mwongozo huu, Jumuiya ya Kimataifa ya Hifadhi ya Jamii haitawajibika kwa namna yoyote kwa data kutokuwa sahihi, kuachwa au makosa yoyote na kiujumla, kwa hasara yoyote ya kifedha au nyingine au uharibifu kwa njia yoyote unaotokana na matumizi ya chapisho hili.

Chapisho hili limeandaliwa kwa kuzingatia taratibu za leseni ya Creative Commons Attribution-NonCommercial-NoDerivs 4.0 Unported License (CC BY-NC-ND 4.0).

Toleo hili lilichapishwa 2024.

ISBN 978-92-843-0149-2

© International Social Security Association, 2017